# KISHINDO CHA TAMISEMI

Toleo Na. 01 | www.tamisemi.go.tz | Juni 10, 2025



# UMITASHUMTA NA UMISSETA 2025 YAFUNGULIWA RASMI

# OFISI YA RAIS, TAWALAZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (OR - TAMISEMI)

ortamisemi

# SAFU YA WACHANGIAJI

1. ANGELA MSIMBIRA - MWANDISHI
2. BRYSON MSHANA- MWANDISHI
3. HUMPHREY KISIKA- MWANDISHI
4. SIMA BINGILEKI -MWANDISHI
5. JANETH MATONDO- MWANDISHI
6. BROWN BOSYE MWANKENJA - MPIGA PICHA
7. JAMES REUBEN-MPIGA PICHA
8. MOHAMED OMARY MIRAJI-MPIGA PICHA
9. JOASH SHAMBA

# TAHARIRI

## HONGERA MHE. RAIS SAMIA SULUHU HASSAN KWA KUBORESHA MICHEZO

Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe.Kassim Majaliwa Majaliwa jana amefungua rasmi mashindano ya Umoja wa Michezo na Taaluma Tanzania yanayofanyika Kitaifa Mkoani Iringa kwa shule za Msingi (UMITASHUMTA ) na Shule za Sekondari (UMISSETA) kwa mwaka 2025 katika viwanja vya Kichangani mjini Iringa.

Michezo ya mwaka huu inajumuisha wanamichezo zaidi ya 7,000 kutoka katika mikoa yote nchini na inaratibiwa na Ofisi ya Rais - TAMISEMI chini ya Waziri Mohamed Omary Mchengerwa ikishirikiana na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia pamoja na Wizara ya Habari, Utamaduni, Utamaduni na Michezo.

Makala ya UMITASHUMTA ya mwaka ni ya 29 na UMISSETA ni ya 45 toka mashindano haya yaanzishwe ambapo katika awamu ya Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan tumeshuhudia mashindano haya yakiboreshwa kila uchao kwa kuongeza michezo mbalimbali na bajeti ya sekta ya Michezo kwa ujumla.

Mathalan, mwaka huu mchezo wa kriketi umejumuishwa.!

Tunampongeza Mhe. Rais kwa kuwa tunaamini michezo hii ni kisima na hazina ya kuzalisha na kuibua vipaji vya wachezaji wa kimataifa katika siku za usoni.

Aidha, tutaendelea kutembea katika maono yake ya kutaka kufungamanisha michezo, utamaduni na utalii ili kuitangaza Tanzania kimataifa hivyo kuliingizia taifa fedha na kuinua uchumi wetu kwa faida ya vizazi vya sasa na baadaye.

**"Mungu ibariki Afrika, Mungu ibariki Tanzania na Mungu mbariki Rais wetu!**



**JOHN MAPEPELE**
**MKUU WA KITENGO CHA MAWASILIANO**
**OR - TAMISEMI**



# MHE. MAJALIWA AFUNGUA UMITASHUMTA & UMISSETA 2025

Na Bryson Mshana

Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe.Kassim Majaliwa, amefungua rasmi mashindano ya Umoja wa Michezo na Taaluma Tanzania yanayofanyika Kitaifa Mkoani Iringa.

Ufunguzi huo wa UMITASHUMTA & UMISSETA 2025 umefanyika katika viwanja vya Kichangani vilivyopo Kata ya Kihesa Manispaa ya Iringa, ukishuhudiwa na wanamichezo zaidi ya 3,000 kutoka katika mikoa mbalimbali nchini.

Amewakumbusha washiriki umuhimu wa kujihusisha na michezo shuleni, kwani licha ya kuwanufaisha kitaaluma lakini pia ni sehemu ya ajira.

"Manufaa ya michezo hii sio ya kitaaluma peke yake, lakini pia michezo ni Ajira, na tunao ushahidi wa wanamichezo wengi katika timu mbalimbali ndani na nje ya nchi, ambao walitokana na mashindano haya, hivyo na nyie mtumie nafasi hii kuonesha vipaji vyenu na hatimaye muonekane kitaifa na kimataifa" ameeleza Waziri Mkuu Majaliwa.

Kuhusu uchaguzi Mkuu ujao, Mhe Waziri Mkuu amesisitiza wanachi kuchagua viongozi wakaojali pia maendeleo ya Taaluma,Michezo pamoja na Sanaa.

Amesema kuwa katika wakati huu ambao Mhe.Rais Dkt.Samia Suluhu Hassan anaendelea kufanya uwekezaji mkubwa kwenye sekta ya michezo nchini, ni vema kuchagua viongozi ambao wataunga mkono kwa vitendo juhudi hizo.

UMITASHUMTA & UMISSETA inaandaliwa na Ofisi ya Rais TAMISEMI ikishirikiana na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia pamoja na Wizara ya Habari, Utamaduni, Utamaduni na Michezo.

Kauli mbiu ya Mashindano ya mwaka huu ni "Viongozi bora ni Msingi wa Maendeleo na Taaluma, Sanaa na Michezo,Shiriki Uchaguzi Mkuu 2025 kwa Amani na Utulivu"



# RC SERUKAMBA ATANGAZA FURSA ZA UWEKEZAJI MKOANI IRINGA KUPITIA MICHEZO

Na Humphrey Kisika na Sima Bingileki

KUFANYIKA kwa Mashindano ya UMITASHUMTA na UMISSETA kitaifa katika Mkoa wa Iringa kunatoa fursa kwa washiriki na wageni kutoka Mikoa yote 26 kutembelea vivutio vya Utalii ndani ya Mkoa wa Iringa na Mikoa ya Jirani.

Kauli hiyo imetolewa na Mkuu wa Mkoa wa Iringa Mhe. Peter Serukamba alipokuwa akitoa salamu za Mkoa kwenye Ufunguzi wa Mashindano ya UMITASHUMTA na UMISETA Kitaifa Katika Mkoa wa Iringa ambayo yanafunguliwa na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa.

Amesema mashindano haya yatafanyika katika viwanja vya Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Iringa,Shule ya Sekondari ya Lugalo na Viwanja vya Chuo Cha Waalimu Kreluu na kuhudhuriwa na zaidi ya wanafunzi 7,000 kutoka Mikoa 26 Tanzania Bara.

Aidha, ameitaja michezo itakayo shindaniwa kiwa ni Soka mpira wa kikapu, mpira wa kemgele, wavu, na Michezo ya fani za ndani ikiwamo ngoma kwaya.

Ufunguzi wa Mashindano ya UMITASHUMTA na UMISSETA Kitaifa katika Mkoa wa Iringa yamehudhuriwa pia na Waziri wa Habari, Sanaa Utamaduni na Michezo Mheshimiwa Palamagamba Kabudi, Ndugu Salim Abri Mjumbe wa Halmashauri Kuu Wabunge, Wakurugenzi wa Wizara, Maafisa wa Wizara, Wanamichezo , Makatibu Tawala na Wakuu wa Wilaya.


25





# DKT. SAMIA AMEONESHA DHAMIRA YA DHATI KATIKA KUBORESHA SEKTA YA MICHEZO NCHINI

Na Mwandishi Wetu

Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo Prof. Palamagamba Kabudi amesema kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe.Dkt.Samia Suluhu Hassan ameonesha dhamira ya dhati katika kuimarisha sekta ya michezo,Sanaa na Utamaduni nchini.

Profesa Kabudi amesema hayo leo Mjini Iringa wakati akitoa taarifa ya Wizara kwenye ufunguzi wa mashindano ya umoja wa michezo na taaluma kwa shule za msingi na Sekondari (UMITASHUMTA & UMISSETA 2025) yanayofanyika Kitaifa Mkoani Iringa.

"Mhe.Rais Dkt.Samia Suluhu Hassan amekuwa mstari wa mbele katika kuinua na kuimarisha michezo nchini, na mifano hai ni uwekezaji mkubwa wa miundombinu ya michezo unaendelea katika shule na vyuo mbalimbali vya elimu nchini" amesisitiza Pro.Kabudi

Ufunguzi wa UMITASHUMTA na UMISSETA 2025 unafanyika rasmi leo Juni 9,2025 ukiongozwa na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe.Kassim Majaliwa.

Kauli mbiu ya mashindano ya mwaka huu inasema "Viongozi bora ni msingi wa maendeleo na Taaluma, Sanaa na Michezo,Shiriki Uchaguzi Mkuu 2025 kwa Amani na Utulivu"


MISSETA
2025





# SERIKALI YA AWAMU YA SITA IMEFANYA JUHUDI KUBWA KUIMARISHA MICHEZO SHULENI

Na Angela Msimbira

Zaidi ya shilingi Bilioni 2.4 zimetengwa kwa ajili ya Mashindano ya Umoja wa Michezo na Taaluma kwa shule za Msingi na Sekondari.

Hayo yameelezwa na Naibu Waziri Ofisi ya Rais-TAMISEMI anayeshughulikia Elimu Mhe. Zainab Katimba wakati wa uzinduzi wa Mashindano hayo kitaifa katika viwanja vya Kichangani kata ya Kihesa Manispaa ya Iringa Mkoani Iringa.

"Nitumie nafasi hii kumshukuru sana Mhe.Rais kwa kuendelea kutuwezesha na kutupatia fedha za kutosha kuandaa na kuendesha mashindano haya kila mwaka, jambo ambalo limeendelea kukuza sekta ya michezo Nchini" Amesema

"Michezo ya UMITASHUMTA na UMISSETA imekuwa na mchango mkubwa katika kuandaa wanamichezo wa timu za Taifa ambao wamekuwa wakiliwakilisha Taifa katika michezo mbalimbali" ameeleza Mhe.Katimba

Aidha Mhe.Katimba amesema kuwa michezo ya shule imekuwa sehemu ya kuimarisha Muungano kutokana na ushiriki wa wanafunzi kutoka Tanzani Bara na Visiwani Zanzibar.

Mashindano ya UMITASHUMTA na UMISSETA inafanyika Mkoani Iringa, ikiwa ni zaidi ya miaka 30 tangu yalipofanyika kwa mara ya mwisho Mkoani humo.


MBEYA


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MKOA WA RUVUMA
UMITASHUMTA
2025



# MICHEZO INAIMARISHA AFYA, AJIRA - WAZIRI MAJALIWA

Na Janeth Matondo

Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Kassim Majaliwa amewataka vijana kuzingatia michezo kwani ni chanzo cha fursa za ajira, inaibua vipaji, inajenga afya na kuongeza uwezo wa kifikiri, inaimarisha nidhamu na uhusiano baina ya wanafunzi.

Mhe. Majaliwa, ameyasema hayo Juni, 09 2025 katika Uwanja wa Kichangani Mjini Iringa wakati akifungua rasmi mashindano ya Umoja wa Michezo na Taaluma Shule za Msingi Tanzania (UMITASHUMTA) na Umoja wa Michezo kwa Shule za Sekondari Tanzania (UMISSETA) kwa ngazi ya kitaifa kwa mwaka 2025.

"Ni matarajio yangu kwenu nyie mtaonyesha jitihada zenu na vipaji vyenu vilivyo bora. Wizara iko hapa, tuna wataalamu hapa wa michezo yote wanaendelea kuwaangalia ubora wenu ili muweze kuchukuliwa katika nyanja mbalimbali muweze kuliwakilisha taifa hili. Kwani michezo inaongeza uwezo wenu, michezo itawafanya mfahamiane, ni fursa ya kuonyesha vipaji, inajenga afya na kuleta matokeo bora kitaaluma". Amesema Majaliwa.

Ametoa rai kwa wizara ya Elimu na TAMISEMI kuimarisha usimamizi wa ratiba za vipindi vya michezo mashuleni, ili kutoa nafasi kwa wanafunzi kushiriki michezo. Vilevile, amewataka watanzania wote kujenga utamaduni wa kufanya mazoezi ya viungo ili kuimarisha afya za watanzania.

Naye, Mkuu wa Mkoa wa Iringa Mhe. Peter Serukamba ambapo mashindano hayo yanafanyika ameishukuru Serikali ya Awamu ya sita kwa kuchagua Mkoa wa Iringa kuwa mwenyeji wa mashindano hayo kwani uwepo wa michezo hiyo ni fursa ya kiuchumi kwa wananchi kwani inaunganisha Iringa na Mikoa ya jirani. Vilevile, itakuza fursa ya utalii







# WAZIRI MKUU AZINDUA MICHEZO YA UMITASHUMTA, ASHIRIKI KUCHEZA

# WASANII WANOGESHA UZINDUZI WA UMITASHUMTA NA UMISSETA






Mashindano ya
UMITASHUMTA
na UMISSETA



Jamhuri ya
ano wa Tanzania




# UMITASHUMTA NA UMISSETA 2025 YAFUNIKA



UMITASHUMTA NA UMISSETA
2025